BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSIANA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS, KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

UTANGULIZI:

Mheshimiwa Spika: Kwanza kabisa, nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mwingi wa Rehema na Mwenye Kurehemu kwa kutujaalia uzima na afya njema ambayo imetuwezesha kukutana tena leo katika siku ya pili ya Baraza hili la Kumi, Mkutano wa Kumi na Moja kwa ajili ya kuendelea na shughuli zetu za kuwatumikia wananchi. Aidha, ninakushukuru wewe binafsi Mheshimiwa Spika na Wasaidizi wako kwa kuliongoza Baraza hili kwa ufanisi mkubwa. Imani yangu ni kwamba mtaendelea kuliongoza Baraza hili kwa weledi na uadilifu wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika: Aidha, napenda kutumia nafasi hii kumshukuru na kumpongeza kwa dhati kabisa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuiongoza nchi yetu kwa uadilifu na kuhakikisha kuwa maendeleo makubwa yanapatikana pamoja na kuendelea kuidumisha hidaya ya Wazanzibari ambayo ni amani na utulivu wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Kamati yetu inampongeza Mheshimiwa Makamu wa Kwanza wa Rais Mheshimiwa Othman Masoud Othman kwa utekelezaji mzuri wa majukumu yake ya kumshauri na kumsaidia Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kutumia hekma na busara ambayo imepelekea kuongezeka kwa uadilifu na weledi wa kusimamia majukumu yao.

Mheshimiwa Spika: Sambamba na hayo, nachukua fursa hii adhimu kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Mheshimiwa Harusi Bint Said Bin Suleiman kwa kuisimamia vyema Wizara hii, sambamba na kuwashukuru watendaji wote wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Ofisi hii Dkt. Omar Dadi Shajak bila kumsahau Afisa Mdhamini Pemba Ndugu Ahmed Abubakar, bila ya kuwasahu watendaji wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa mashirikiano yao waliyoyaonyesha wakati wa kupitia makadirio ya Bajeti ya Ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Spika: Aidha, shukurani za pekee ziwaendee Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati kwa jinsi yunavyoshirikiana katika kutekeleza majukumu ya Kamati yetu na kuhakikisha kuwa thamani halisi ya fedha inapatikana katika utekelezaji wa kazi za Wizara hii kwa kila Taasisi husika.

Mheshimiwa Spika: Kwa heshima na taadhima, naomba sasa kuwatambua Wajumbe hao kwa majina kama ifuatavyo:

1.	Mhe. Machano Othman Said	Mwenyekiti
2.	Mhe. Mtumwa Peya Yussuf	Makamu Mwenyekiti
3.	Mhe. Suleiman Makame Ali	Mjumbe
4.	Mhe. Salma Mussa Bilal	Mjumbe
5.	Mhe. Mohamed Mgaza Jecha	Mjumbe

6.	Mhe. Zaina Abdulla Salum	Mjumbe
7.	Ndg. Ali Alawy Ali	Katibu
8.	Ndg. Mwanaisha Mohammed Kheir	Katibu, na
9.	Ndg. Amina Abeid Hemed	Mkalimani

Mheshimiwa Spika: Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa imepitia na kujadili jumla ya mafungu Manne (04) ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ambayo yameletwa mbele ya Kamati hii, mafungu wenyewe ni B01 – Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Ofisi Kuu; B04 – Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira; C04 – Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya; na Fungu C05 – Tume ya UKIMWI, ambapo lengo kuu ni kujadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ya mwaka wa fedha 2023/2024.

FUNGU B 01: **OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS**

Mheshimiwa Spika: Kiujumla Kamati imeridhishwa na utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 ambapo ilifanikiwa kwa asilimia kubwa kufikia malengo yaliyopangwa kwa program zake kuu na ndogo na hivyo kuweza kuimarisha hali ya ustawi wa wananchi na mazingira ya asili. Hivyo, kwa mwaka huu Ofisi inategemea kutekeleza Programu kuu *tatu (3)* ambazo ni Programu ya Usimamizi wa Mazingira, Uratibu wa Mabadiliko ya Tabianchi, Programu ya Watu wenye Ulemavu na Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais. Maelezo ya kina ya programu hizo yametolewa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri pamoja kitabu cha Bajeti cha makadirio ya mapato na matumizi ya fedha cha mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Spika: Kupitia program ya **Uratibu wa Mabadiliko ya Tabianchi** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ofisi imepanga kuipitia sera ya mazingira ya

mwaka 2013, kupitia Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2025 pamoja na mambo mengine yanayohusu tafiti kuhusu maeneo yaliyoathirika na mabadiliko ya Tabianchi kisiwani Pemba. Kamati inaunga mkono malengo haya na haina shaka na utekelezaji wa mipango hii bali tunaishauri Ofisi ya Makamu wa Kwanza kusimamia kikamilifu utekelezaji wa mipango hii kwa kupatiwa fedha kama zilivyoainishwa katika bajeti yake.

Mheshimiwa Spika: Kamati yangu pia, imeridhishwa na maendeleo ya Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu kutokana na uwezeshaji unaofanywa kupitia program mbali mbali za kuinua ustawi wa watu wenye ulemavu Zanzibar. Aidha, Kamati inaishukuru Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa kuratibu vyema programu ya Masuala ya Watu wenye Ulemavu Zanzibar na kuhakikisha Sheria na Taratibu za nchi zimefuatwa ili kuondosha unyanyasaji wa watu wenye ulemavu katika jamii.

FUNGU B04: MAMLAKA YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA

Mheshimiwa Spika: Kamati inatoa pongezi kwa Mamlaka ua Usimamizi wa Mazingira Zanzibar kwa kuvuka malengo yake ya ukusanyaji wa mapato jambo ambalo linaleta faraja kwa Kamati na Serikali kwa ujumla. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Mamlaka hii imeongezewa makadirio ya kiwango cha ukusanyaji wa mapato kwa takribani asilimia 90% kwa mwaka sawa na asilimia 130 ya makusanyo kwa miezi tisa ambapo imepelekea kutoka TSH. Milioni 300 ya mwaka 2022/2023 na kupangiwa TSH. Milioni 574 kwa bajeti ya mwaka 2023/2024. Hii ni hatua kubwa ya mafanikio ambayo imefikiwa kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira kwa upande wa uimarishaji wa mapato. Kamati inaishauri Mamlaka kuzidisha kasi ya ukusanyaji wa mapato pamoja na kuendeleza mapambano dhidi ya uhifadhi mazingira na kuinusuru nchi yetu kutokana na athari za mabadiliko ya Tabianchi.

Mheshimiwa Spika: Aidha, kupitia programu **kuu ya Usimamizi wa Mazingira,** Kamati inaiomba Mamlaka kuimarisha shughuli za mazingira kwa kutoa elimu na miongozo kwa jamii juu ya umuhimu wa kuhifadhi mazingira sambamba na kuweka mikakati itakayoisaidia jamii kushiriki kikamilifu katika zoezi la upandaji miti hususan upandaji wa mikoko katika sehemu za pembezoni mwa bahari. Kamati pia, inaishauri Mamlaka kuanza kuishawishi jamii kuhifadhi mazingira kupitia mradi wa biashara ya kaboni ili kuwanufaisha kwa kipato lakini pia kusimamia matumizi endelevu ya mazingira.

Mheshimiwa Spika: Kamati yangu inaishauri Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kupitia programu ndogo ya *Tathmini na Ufuatiliaji wa Kimazingira* kuhakikisha tathmini imefanyika kwa maeneo yote ambayo yameathirika na yanaendelea kuathirika kutokana na mabadiliko ya Tabianchi, maeneo kama vile Kisiwa Panza, Ndagoni na Kojani kwa upande wa Pemba na eneo la Jambiani kwa upande wa kusini Unguja. Kamati inataka kuona ni kwa kiasi gani suala la usimamizi endelevu wa mazingira na maliasili umekamilika na kumfikia kila mmoja ili kuifanya jamii ifahamu kuwa changamoto za kimazingira zinasababishwa na matumizi ya mazingira na maliasili yasiyo sahihi katika maeneo husika.

FUNGU C04: **MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA ZANZIBAR**

Mheshimiwa Spika: Kupitia programu kuu ya Udhibiti wa dawa za kulevya; Kamati yangu inampongeza Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar kwa juhudi zake anazochukua kupambana na wahalifu wa dawa za kulevya Zanzibar. Kamati inaamini kwamba kufanikiwa kwa Mamlaka katika kutekeleza majukumu yake ni kufanikiwa kwa Serikali katika kupinga matumizi ya dawa za kulevya hapa nchini.

Mheshimiwa Spika: Kwa mnasaba huu, Kamati imepata wasiwasi kuona kiwango cha fedha kilichopangwa kupitia program ndogo ya *Uchunguzi, Operesheni wa Dawa za Kulevya na Uhalifu Unaofana nao* haitofanyika kwa ufanisi kutokana na kupangiwa fedha ndogo ambayo ni jumla ya TSH Milioni 68 tu ikizingatiwa kwamba vitendo hivi ni vya kila siku na operesheni hizi zinahitajika kufanyika kila siku. Hivyo hivyo, kupitia program kuu yenyewe ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya imepangiwa kiasi cha THS. Biloni 1.8 tofauti na mwaka uliopita ambapo ilipangiwa kiasi cha TSH. Biloni 4.00 maana yake kazi hii itaenda kuwa ngumu zaidi kutokana na uhaba wa fedha ambao tumempa Kamishna wa Mamlaka hii.

Mheshimiwa Spika: Mafanikio chanya yatapatikana endapo Serikali itaweka nguvu zake katika mapambano dhidi ya Dawa za Kulevya kwa kuimarisha rasilimali fedha na rasilimali watu, kuimarisha mifumo ya ulinzi wa baharini na nchi kavu; vitu ambavyo ndio nyenzo muhimu katika mapambano na kufikia malengo. Hata hivyo, juhudi zote zinazofanyika haziwezi kutimiza malengo ikiwa Mamlaka itakua mbali na wananchi na kwa maana hiyo Mamlaka iwekeze nguvu maalumu ambayo itaifanya jamii kutoa taarifa za kihalifu wakati wote ambao watu waovu wanatekeleza harakati zao.

Mheshimiwa Spika: Kamati yangu imepata amani kuona kwamba kwa mwaka huu Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya imepangiwa mradi ambao utaimarisha Mamlaka kwa kufanya ununuzi wa vifaa vya kisasa pamoja na kuboresha huduma za ustawi wa jamii na upatikanaji wa huduma bora na endelevu. Kamati imeridhishwa na kiwango cha fedha za mradi zilizopangwa katika makadirio ya mwaka 2023/2024 isipokuwa tunaishauri Serikali fedha zilizopangwa katika bajeti ya 2022/2023 ambazo zimepatikana kwa asilimia ndogo, fedha zilizobakia zipelekwe katika Mamlaka ili zikatumike kwa malengo yaliyokusudiwa kwani program iliyokusudiwa kutekelezwa kupitia fedha hizo za mradi haijakamilika.

FUNGU C05: TUME YA UKIMWI

Mheshimiwa Spika: Fungu C05 linasimamia program kuu mbili ambazo ni program ya kuratibu muitiko wa Taifa wa UKIMWI na program ya Utumishi na uendeshaji. Ni jambo la faraja kuona kuwa makadirio ya bajeti ya mwaka 2023/2024 yamezingatia vyema maelekezo ya Serikali ya kuimarisha huduma za afya ikiwemo VVU na UKIMWI na kwenda sambamba na vipaumbele vya kuimarisha miundombinu ya bandari, barabara na viwanja vya ndege. Aidha, Tume ina wajibu wa kujiwekea mkakati maalumu ambao utaiwezesha kujiendesha kama taasisi yenye kutoa huduma badala ya kusubiri ruzuku na misaada kwa ajili ya kujiendesha.

Mheshimiwa Spika: Kamati pia, inaitaka Tume kuzidi kufanya kazi kwa umakini mkubwa na kwa kuzingatia uadilifu, sambamba na kuzifuatilia Jumuiya zote zinazojihusisha na mapambano dhidi ya UKIMWI na kuona hatua wanazochukua juu ya mapambano haya kwa kufahamu malengo na mikakati ya kila Jumuiya, kufahamu wafadhili wa Jumuiya hizi pamoja na kuzipa ushauri wa namna ya kujenga mashirikiano na jamii. Aidha, Kamati pia inaishauri Serikali kuongeza Fungu la Fedha la C05 kwa Tume ya Ukimwi ili kupunguza utegemezi wa wafadhili wa nje.

HITIMISHO:

Mheshimiwa Spika: Mwisho, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni yetu, kwa niaba ya Kamati pamoja na kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kunisikiliza kwa umakini wakati wote wa uwasilishaji wa maoni ya haotuba hii. Aidha, Kamati inatoa ombi maalumu kwa Serikali na kufikiria kwa makini kuipatia fedha za kutosha Mamlaka ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya Zanzibar kwa ajili ya kwenda sambamba na mabadiliko ya Ulimwengu na kwasababu waathirika wakubwa ni vijana, na vijana ndio msingi wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika: Mwisho kabisa, ili kufikiwa malengo yaliyopangwa katika utekelezaji wa majukumu yake, Kamati inawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu waichangie, wairidhie Bajeti hii na hatimae waidhinishie Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais makadirio na makisio ya fedha zote zilizopangwa kutumiwa kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ili waweze kutekeleza majukumu yao kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika: *kwa niaba ya Kamati yangu*

Naomba Kuunga Mkono Hoja!

Ahsante,

.....

(Machano Othman Said)

Mwenyekiti,

Kamati ya Kudumu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa,

BARAZA LA WAWAKILISHI,

ZANZIBAR.